سواحلي

*Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu*

# Qur-ani Tukufu ni nini?



Qur-ani Tukufu ni maneno ya Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote na Muumba wao. Aliiteremsha juu ya yule wa mwisho wa Manabii na Mitume, Muhammad rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Ili, awabainishie wanadamu malengo ya kuumbwa kwao, na ili kuwaongoza kuyaendea yale yaliyomo furaha yao katika dunia na Akhera. Na ili kuwatoa kutokana na taabu ya milele baada ya kifo. Nacho ndicho Kitabu cha mwisho kuteremka miongoni mwa vitabu vya Mwenyezi Mungu. Chenye kuvisadikisha (vitabu hivyo), na chenye kufuta sharia zavyo.

Na Qur-ani Tukufu ni Aya (ishara) na ni muujiza wa milele. Nayo ni ushahidi juu ya unabii wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Muhammad rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Mwenyezi Mungu aliwapa changamoto watu na majini kwamba walete mfano wake (Qur-ani), bali hata sura moja tu itokanayo na Qur-ani, lakini wakashindwa kufanya hivyo.

Qur-ani haikufikiwa na mkono wa upotoshaji na ubadilishaji tangu kuteremka kwake kabla ya zaidi ya miaka 1400. Na itabaki imehifadhiwa kwa lugha ya Kiarabu ambayo iliteremka kwayo. Kwani, Mwenyezi Mungu, Utakatifu ni wake, Mtukufu alichukua dhamana ya kuihifadhi mpaka zama za mwisho.

Na Qur-ani Tukufu ndiyo chimbuko kuu la Uislamu, na katiba ambayo inapangilia maisha ya wanadamu. Na inayohukumu katika kila zama na sehemu. Inalingania katika kumwabudu Mungu, Muumbaji peke yake. Na inabainisha kile anachohitaji mwanadamu ili kumjua Mola wake Mlezi na dini yake na mwanzo wa uumbaji wa ulimwengu, na awamu za uumbaji wa mwanadamu. Na anajulisha kuhusu ghaibu zilizopita na zijazo. Na kuhusu visa vya Manabii waliopita, amani iwe juu yao, na namna Mwenyezi Mungu alivyowanusuru na akawaangamiza maadui wao. Na ndani yake kuna misingi ya ibada zote, na miamala, na kulingania katika tabia njema, na kutahadharisha na tabia mbaya, na maishio ya mambo huko Akhera, ima Pepo; Nyumba ya Waumini, na ima Moto; Nyumba ya madhalimu na makafiri.

Na kwa sababu ya umuhimu wa Kitabu hiki kitukufu ambacho Mwenyezi Mungu alikiteremsha kwa lugha ya Kiarabu, na akaamrisha kifikishwe kwa wanadamu, inatufurahisha sisi - ewe msomaji mtukufu - tukuletee tarjama ya maana yake kwa lugha yako; ili kurahisisha kuifahamu (Qur-ani hii) na kuhakikisha kuifikisha kwake. Na bila shaka. jopo kazi limefanya jitihada yake katika kufahamu maana zake, kuifanyia tarjama, pamoja na kujua kwa yakini kwamba hata tarjama ikifikia kiwango kipi cha usahihi, itabaki kuwa na mapungufu katika kueleza maana kubwa ambazo Qur-ani Tukufu inaziashiria katika maandiko ya Qur-ani Tukufu, yenye ushindi, ambayo yanashinda kazi yoyote ile ya kibinaadamu. Na atakayetaka kupata ziada ya hakika zilizoletwa na Qur-ani Tukufu, basi tunamuusia ajifunze lugha ya Kiarabu ambayo iliteremka kwayo.

**Unaweza kuona tarjama ya maana za Qur-ani Tukufu katika lugha yako kupitia msimbo wa (QR)**

**Inatufurahisha kupokea mapendekezo yenu na maangalizo yenu, kwa ajili ya kuboresha tarjama hii kupitia dirisha la maangalizo linalopatikana mbele ya kila aya; kupitia tovuti ya ensaiklopidia ya Qur-ani Tukufu**

**www.quranenc.com**

موسوعة القرآن الكريم
QuranEnc.com

**Na ukitaka kuwasiliana nasi, basi inawezekana kututumia ujumbe kupitia barua pepe**

**info@quranenc.com**

**www.islamHouse.com**